USAFI NA CHANJO

Na Augustino Chengula

Zipo njia kuu mbili zinazotumika ili kusaidia kuzuia maonjwa ya kuku yasiwapate kuku wako. Njia ya kwanza ni ya kuzingatia usafi katika banda na mazingira yanayozunguka banda, nay a pili ni kwa kuchanja kuku wako kila inapobidi.

1. Usafi wa banda na mazingira yake

Kabla ya kununua kuku au vifaranga hakikisha mambo yafuatayo yanazingatiwa;

i. Hakikisha shamba lako limejitenga kutoka kwa wafugaji wengine ili kupunguza maambukizi kutoka kwa kuku wa jirani yako.

ii. Hakikisha nyumba au banda la kuku limejengwa eneo ambalo kuna hewa ya kutosha ili kusaidia kuku wako wasipate magonjwa ya mfumo wa upumuaji. Kivuli pia kwa kuku ni vema kikazingatiwa na kama ni mabanda ya wazi basi yajengwe kwa ulekeo wa mashariki kwa magharibi ili kukinga jua.

iii. Hakikisha shamba lako halirusi watu kuingia ovyo au kuwa na nafasi ya kuona kuku wako kirahisi kwa hofu ya maambukizi toka huko wanakotoka

iv. Vifaa vya kuku viwe vinasafishika kwa urahisi, fanya uchaguzi mzuri ili visitunze uchafu utakao vuta vimelea vya magonjwa vizaliane na kusababisha magonjwa kwa kuku.

v. Wafanyakazi wa kuku lazima wawe na nguo, viatu maalumu kwa kazi ya kuku na hata wageni au wataalamu wa mifugo wapewe viatu vingine waingiapo ndani ya banda kupunguza maambukizi toka mashamba mengine

vi. Karibu na mlango wa kuingilia tengeneza kijisehemu cha kuweka dawa ambapo waingiaji ndani ya banda watakanyaga na watokapo ili kama kuna wadudu kwenye viatu vyao wasiingie ndani ya banda wala wasitoke ndani ya banda.

vii. Hakikisha wadudu na wanyama kama panya, nyoka, ndege wa polini hawaingii ndani ya banda maana wanaweza kuleta magonjwa na kula kuku/vifaranga wako na kukurudisha nyuma.

viii. Siku zote tumia malalia ya kuku yaliyo safi (maranda ya mbao, pumba ya mpunga) na badilisha mara yanapokuwa na unyevu ili uzuia maambukizi ya magonjwa. Maranda ya mbao zilizowekwa dawa hayafai kutumika kwani yanaweza kuwa sumu kwa kuku.

Usafi- Usafi ndani ya banda ni kinga ya kutosha kwa maambukizi ya magonjwa, hakikisha banda lako kila siku linakuwa safi. Kuku wakifugwa kwa njia ya keji ni rahisi kufanya usafi na hivyo maambukizi kwa kuku huwa si rahisi kama ufugaji wa chini. Mra unapouza kuku wote ndani ya banda basi kabla hujaleta kuku wengine hakikisha usafi wa kina unafanyika na kupulizia dawa, kasha liache kwa muda kuanzia mwezi mmoja hivi ili uwe na uhakika wadudu wote wa magonjwa waliotokana na ufugaji uliopita wanakufa.

2. Uchanjaji wa kuku

Chanjo ni kinga wanayopewa kuku ili waweze kukabiana na vimelea vya magonjwa mbalimbali na hatimaye kuku wasipate magonjwa hayo. Kiuhalisia chanjo nyingi zinafanana sana na wadudu wanaosababisha magonjwa husika na baadhi huwa zimetengenezwa kutokana na sehemu ya mdudu yule. Zipo chanjo ambazo zinatengenezwa kutokana na wadudu walio hai lakini wakiwa wamepunguzwa

makali ili wasimdhulu kuku na nyingine zinatokana na wadudu waliouawa au sehemu tu ya yule mdudu kwa malengo yale yale ya kutomdhulu kuku.

Chanjo ikifika ndani ya mwili wa kuku inachokifanya ni kuongeza kinga ya mwili kwa ugonjwa unaosababishwa na mdudu aliye tengezea chanjo ile. Hivyo kuku aliyechanjwa na chanjo hiyo atakingwa na wadudu wa ugonjwa huo tu, kwani kinga ile itapambana na wale wadudu wakiingia mwilini na kuwateketeza ili wasimletee ugonjwa yule kuku. Hivyo ukichanja kuku wako kwa chanjo fulani hutakuwa umezuia magonjwa yote, ni kwa ugonjwa husika tu. Labda kwa baadhi ya chanjo ambazo zimechanganywa wadudu tofauti, wawili au watatu, hizo zinaweza kupambana na magonjwa hayo mawili au matatu lakini si yote.

Kuku wanaanza kuchanjwa kutegemea na ugonjwa gani unataka kuwakinga nao, yaweza kuwa siku wanayozaliwa, wiki moja, mbili au zaidi. Hii inategemea na kinga ya mototo/kifaranga anayoipata toka kwa mama inauwezo wa kukaa kwa muda gani ndani ya mototo kulingana na ugonjwa inaomkinga hiyo kinga ya mama. Hata ukichanja kuku, inategemea chanjo hiyo inauwezo wa kutengeneza kinga inayokaa kwa muda gani ndani ya kuku. Chanjo ya wadudu walio hai inanguvu zaidi na kinga yake huwa ya muda mrefu zaidi, lakini kuna wakati yaweza kuleta ugonjwa kwa kuku (mara chache sana).

Jedwali hapa chini linaonyesha lini unatakiwa kuanza kuchanja kuku wako na kwa ugonjwa gani.

a. Wazazi

Hawa ni kuku kwa ajili ya kuzaa kuku wa kutaga mayai na kuku wa nyama.

Umri wa kuku	Chanjo	Njia ya uchanjaji

Siku 1	Chanjo ya Mareksi	Sindano kwenye nyama
Siku 3-10	Chanjo ya Gumboro	Kwenye maji ya kunywa na matone machoni
Wiki ya 3	-Chanjo ya Kideli (Newcastle) -Chanjo ya Mareksi -Chanjo ya maambukizi ya Mkamba (Bronchitis)	Kwenye maji ya kunywa
Wiki ya 8	-Chanjo ya Kideli Chanjo ya Mkamba	-Kwenye maji ya kunywa -Maji ya kunywa/kwa kunyunyiza
Wiki ya 10	Chanjo ya Gumboro	-Kwenye maji ya kunywa
Wiki ya 14	Uvimbe wa ubongo na neva kuu (Avian encephalomyelitis)	-Kwenye maji ya kunywa
Wiki ya 16	-Chanjo ya Kideli, Mkamba, na Gumboro	-Kuchoma sindano kwenye nyama

b. Kuku wa nyama (kwa biashara)

-Hawa wanafugwa kwa wiki 7

-Wanaweza kupata kirahisi magonjwa ya mfumo wa upuaji kwa sababu hurundikwa wengi ndani ya banda.

Umri wa kuku	Chanjo	Njia ya uchanjaji
Siku 1	-Chanjo ya Kideli -Chanjo ya Mkamba (Infectious	-Kunyunyiza (wanakozalishiwa)

	Bronchitis)	-Kunyunyiza
Siku 3	Chanjo ya Gumboro	Kwenye maji ya kunywa na matone machoni
Wiki ya 18	-Chanjo ya Kideli -Chanjo ya Mkamba	-Kwenye maji ya kunywa -Maji ya kunywa

Chanjo nyingine zipo pia kwa magonjwa kama Ndui ya kuku (Fowl pox), Coryza na Maikoplasma, na zinategemea na tishio la haya magonjwa eneo husika. Shauriana na daktari wako ili kujua ni yapi yanafaa kuchanja.

c. Kuku wa mayai

Kuku wanofugwa kibiashara kwa lengo la kutaga mayai wanahitaji kupewa chanjo zote muhimu kulingana na eneo ukilinganisha na kuku wa nyama.

Umri wa kuku	Chanjo	Njia ya uchanjaji
Siku 1	Chanjo ya Mareksi	Sindano kwenye nyama
Siku 3-10	Chanjo ya Gumboro	Kwenye maji ya kunywa na matone machoni
Wiki ya 3	-Chanjo ya Kideli (Newcastle) -Chanjo ya maambukizi ya Mkamba (Infectious Bronchitis)	Kwenye maji ya kunywa/kwa kunyunyiza
Wiki ya 7	-Chanjo ya Kideli Chanjo ya Mkamba	-Maji ya kunywa/kwa kunyunyiza
Wiki ya 10	Uvimbe wa ubongo na neva kuu (Avian	-Kwenye maji ya kunywa

	encephalomyelitis)	
Wiki ya 14	-Chanjo ya Kideli -Chanjo ya Mkamba -Chanjo ya urabikaji wa mayai	-Kuchoma sindano kwenye nyama

Kushindwa kwa chanjo kufanya kazi

Kuna uwezekano ukachanja kuku wako nab ado wakaugua, na hii inaweza kusababishwa na mambo yafuatayo;

i. Kutotunza vizuri kufuatana na maelekezo ya mtengenezaji mfano kutoweka katika ubaridi ulioainishwa, lakini pia chanjo inaweza kuchakachuliwa na maji.

ii. Uchanjaji ukifanyika wakati kuku tayari na ugonjwa

iii. Chanjo pia yaweza kuwa si ya aina ya mdudu yule halisi wa eneo lako hata kama ni ugonjwa ule

iv. Kuku wakiwa katika mazingira ya mfadhaiko/msongo uliosababishwa na mabadiliko ya kimazingira, uhaba wa chakula, magonjwa mengine n.k, wakati wa uchanjaji wanaweza wasitengeneze kinga inayokusudiwa

v. Upungufu wa kinga unaotokana na magonjwa kama Gumboro na Mareksi utasababisha kuku wasitengeneze kinga kwa ugonjwa unaokusudia kuwakinga.